

**MAELEZO YA MRADI WA BARABARA YA TANGA -
HOROHORO YALIYOTOLEWA NA KATIBU MKUU
WA WIZARA YA MIUNDOMBINU, ENG OMAR A.
CHAMBO, WAKATI WA HAFLA YA UZINDUZI RASMI
WA UJENZI WA BARABARA YA TANGA -
HOROHORO TAREHE 28 MEI 2010**

**Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,**

**Mheshimiwa Dkt Shukuru Jumanne Kawambwa
(Mb), Waziri wa Miundombinu,**

**Mheshimiwa Alfonso E. Lenhardt, Balozi wa
Marekani nchini Tanzania,**

Mheshimiwa Daniel Wolde Yohannes, Mtendaji

Mkuu wa mfuko wa changamoto za Millenia (MCC)

Mheshimiwa Meja Jenerali Mstaafu Said Kalembo

Mkuu wa Mkoa wa Tanga,

Waheshimiwa Wageni Waalikwa Mabibi na

Mabwana.

Mhe. Rais,

1. Naomba kutoa taarifa fupi ya mradi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Tanga hadi Horohoro ambayo muda mfupi ujao utazindua rasmi.

Mheshimiwa Rais,

2. Barabara ya Tanga hadi Horohoro ina urefu wa kilometa 65. Barabara hii inaunganisha Tanzania na Nchi jirani ya Kenya. Mradi wa ujenzi wa barabara hii unagharamiwa na Serikali ya Marekani kupitia Mfuko wa Changamoto za Millenia (MCC).

Mheshimiwa Rais,

3. Mkataba wa Ujenzi wa barabara ya Tanga hadi Horohoro ulitiwa saina tarehe 22 Desemba 2009 kati ya **Mtendaji Mkuu - Mfuko wa Maendeleo ya Milenia - Tanzania** kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kampuni ya **Sinohydro Corporation Limited** kutoka

nchini China. Mkataba wa ujenzi wa barabara hii ni wa miezi 27. Hivyo mradi huu utakamilika Aprili 2012.

Katika ujenzi wa barabara hii Mkandarasi anasimamiwa na Kampuni ya Intercontinental Consultant ya India.

Mheshimiwa Rais,

4. Serikali ya Marekani kupitia Mfuko wa changamoto za Milenia itagharamia ujenzi wa barabara pamoja na usimamizi wa kazi.

Jumla ya shilingi bilioni 69.9 zitatumika kwa ujenzi na shilingi bilioni 3.0 zitatumika kwa kazi za usimamizi.

Serikali ya Tanzania inagharamia ulipaji fidia kwa wananchi ambao imelazimu kupisha ujenzi wa

barabara hii. Aidha, Serikali ya Tanzania imejenga nyumba za Ibada zilizokuwa kwenye eneo la Mradi. Jumla ya misikiti mipya 21 na madrasa 5 zimejengwa na kukabidhiwa kwa wananchi. Serikali ya Tanzania inagharamia pia uhamishaji wa miundombinu ya umeme, maji na simu kutoka katika eneo la ujenzi wa barabara. Jumla ya shilingi bilioni 5.15 zimetumika. Hivyo ujenzi wa barabara hii (kutoka Tanga hadi Horohoro) utagharimu jumla ya shilingi 78.05 bilioni.

Mheshimiwa Rais,

5. Usanifu wa barabara hii ulifanywa kwa kuzingatia viwango vifuatavyo:

- Upana wa barabara ni meta 9.5 ambao unajumuisha meta 6.5 za njia ya magari na meta 1.5 za mabega ya barabara kila upande.
- Barabara hii itajengwa kuanzia kwenye tabaka la mwanzo (*Subgrade*), likifuatiwa na tabaka la kwanza la msingi wa barabara litakalochanganywa kwa saruji na changarawe (*Cement stabilized sub base*).
- Tabaka hilo litafuatiwa na tabaka la msingi wa barabara ambalo litajengwa kwa mawe ya kusaga (*crushed stone base course (CRR)*) na juu yake litafuatiwa na tabaka moja la zege ya lami (*Asphalt Concrete*) kwenye eneo la njia ya magari pamoja na mabega yake.
- Daraja moja lenye urefu wa meta 39 litajengwa.

- Jumla ya makaravati makubwa yapatayo 51 yenye milango 2 hadi 4 yatajengwa.
- Makaravati ya kawaida 102 yenye ukubwa wa kuanzia kipenyo cha meta 0.9 mpaka 1.2 yatajengwa.
- Alama zote za kutahadharisha, kuelekeza na kuongoza magari zinazokidhi viwango vya kimataifa zitawekwa wakati wa ujenzi
- Aidha kutakuwa na njia za mchepuko zitakazokidhi viwango vya kimataifa vya ujenzi wa barabara ili kupunguza msongamano wakati wa kipindi cha ujenzi.

MHESHIMIWA RAIS NAOMBA KUWASILISHA